Jarida la Shirika, Uimarishaji Mifereji Asili na Hifadhi ya Mazingira

Maendeleo ya TIP

Toleo la 4 Julaiy 2003

WAKULIMA NA MASOKO

TIP imekuwa ikifanya kazi kwa kutumia kifurushi chake. Kifurushi cha TIP kina sehemu tatu. Uimarishaji vikundi na Jinsia,Umwagiliaji na Uhifadhi wa udongo na maji. Uzalishaji katika maeneo ambayo TIP imefanya kazi na wakulima umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kutokana na kuongezeka kwa uzalisha tatizo la masoko likawakabili wakulima. Kukawa na ushindani wa kibiashara katika masoko ya ndani.

TIP katika malengo yake ya kuinua wakulima wadogo kiuchumi imeona tatizo hili na ili kulitatua ikaamua kuongeza sehemu nyengine katika kifurushi chake cha "**Kuwawezesha wakulima wadogo kuunda vikundi vya uzalishaji na masoko**".

Mradi wa majaribio wa kuviwezesha vikundi 3 vya watumia maji vya Lushoto unaojulikana kama BAPPA (Beyond Agricultural Productivity to Poverty Alleviation) ulianzishwa kwa ushirikiano kati ya TIP na CIAT (International Centre for Tropical Agriculture). Matokeo yake yameiwezesha TIP kutengeneza mtiririko wa hatua kwa hatua zitakazowawezesha wakulima wadogo kuunda vikundi vya uzalishaji na kuweza kukabiliana na masoko katika maeneo yale ambayo TIP inafanya kazi.

Malengo:

- Kuwawezesha wakulima wadogo kuuza mazao kwa faida
- Kuwawezesha wakulima kuchagua kulima mazao yenye faida
- Kujaribu mbinu au njia za kuwawezesha wakulima kuwa wabunifu

Mafanikio:

Ushirikiano uliopo kati ya TIP na CIAT/BAPPA umefanikisha kuwawezesha wakulima katika kufanya utafiti wa masoko, kufanya maamuzi ya bei ya zao husika, mafunzo ya kilimo bora, kuunda vikundi vya uzalishaji, kufanya majaribio pamoja na kutembelea vikundi ambavyo vinafanya vizuri katika masoko.

Kwa mafanikio yaliyopatika na kwa vikundi 3 vya wakulima wa Lushoto, TIP itatumia utaalamu ule ule ili kufanikisha wakulima wengine waliopo kwenye maeneo ambayo TIP hufanya kazi.



Mwenendo mzuri wa mawasiliano katika ushirikishwaji

Yaliyomo

Mtandao wa TIP	**2**
Changamoto	**2**
Ukarabati wa mfumo wa.....	**3**
Shukrani	**3**
Kazi za TIP kwa Idara	**4**

MTANDAO WA TIP

Shirika La Uboreshaji na Uimarishaji Mifereji ya Asili na Hifadhi ya Mazingira ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa kisheria mwezi wa Agusti 1999. Mtazamo wa shirika ni kuwa rafiki wa karibu wa wakulima wadogo katika kuwawezesha kuinua uchumi wao kwa kuihusisha jinsia na katika matuizi ya umilikishaji wa ardhi na maji.

TIP hutoa huduma kwa wadau wa umwagiliaji wa asili wa Wilaya za Lushoto, Same, Mwanga, Arumeru na wilaya mpya kwa TIP za Hai na Moshi Vijijini.

Kwa niaba ya Halmashauri za Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya husika husaini mkataba wa ushirikiano na Mkurugenzi wa TIP kila mwaka. Kwa kufuatia mkataba wa ushirikiano, kazi za TIP wilayani hufanywa na wafanyakazi wa halmashauri waliochaguliwa kulingana na matakwa ya TIP isipokuwa kwa wilaya ya Moshi Vijijini, kazi huhutekelezwa moja kwa moja kutoka Ofisi kuu ya TIP-Moshi

WAJUMBE WA BODI

1. Prof. S. A. Chambo – M/kiti wa Bodi (Mkuu wa Chuo cha Ushirika - Moshi)
2. Bi. B. Kinabo – Makamu Mkiti wa Bodi (Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Arumeru)
3. Bi. E. Minde – Mjumbe (Mwanasheria)
4. Prof. E. Lazaro – Mjumbe (Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Cha Kilimo cha Sokoine - Morogoro)
5. Dr. B. Koda – Mjumber (Profesa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)
6. Dr. F. Lerise – Mjumbe (Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Ardhi)
7. Eng. R. Temu – Mhandisi ASBS,Wizara ya Kilimo
8. Bw. B. Makau – Mjumbe,(Mkulima Wilaya ya Lushoto)
9. Bw. S. Loti – Mjumbe (Mkulima, Wilaya ya Arumeru)

WAFANYAKAZI WA TIP

OFISI KUU

- Mkurugenzi Mtendaji – Dr. I.H. Kawa
- Mshauri wa Umwagiliaji - Eng. Jan Moijes
- Mhandisi wa Umwagiliaji – Eng. Anenmose Maro
- Afisa Jinsia na Uimarishaji Vikundi – Bi. Shangwe Kiluvia
- Afisa Mipango Ardhi –Bw. Peter Mjata
- Afisa Utawala na Fedha – Bw. Suitbert Mumburi
- Afisa wa Masoko na Mafunzo – Bi. Eva Kassara
- Mtunza Takwimu – Bw. Fokas Makauki (Mkataba wa muda)

WAFAYAKAZI WENGINE

- Katibu Muhtasi Kiongozi – Bi. Zaina Kadege
- Katibu Muhtasi – Bi. Jane Munuo
- Mnadhifu – Bi. Lina Mkeni
- Dereva na Fundi Makanika – Bw. S. Sufi
- Madereva – Bw. G. Tebe, Bw. M. Mbigili na Bw. D. Sulley, Bw. H. Lagya - (Mkataba wa muda)
- Mtunza Bustani – Bw. P. Kiwale

CHANGAMOTO

Mashirika yasiyo ya kiserikali kama shirika la Uimarishaji wa Mifereji ya Asili na Hifadhi ya Mazingira (TIP) yametakiwa kushirikiana kwa pamoja na wataalamu wa halmashauri za wilaya wakati wa utoaji wa mafunzo/elimu ya miradi endelevu kwa wakulima.

Changamoto hiyo imetolewa na Bi. Elizabeth Minde (Mwanasheria na Mjumbe wa Bodi ya TIP) wakati akifunga semina ya wiki mbili iliyofanyika Moshi ili kutoa mafunzo kwa maofisa wa TIP na washirika wa TIP katika halmashauri za wilaya ya Lushoto, Same, Mwanga, Arumeru na Moshi Vijijini kuhusu mbinu za uwezeshaji katika kuwaendeleza wanawake na wanaume kwenye miradi yao ili iwe endelevu. Kutoka katika gazeti la Majira la Octoba 7, 2002

MTANDAO WA TIP WILAYANI

UMWAGILIAJI			
ARUMERU	**MWANGA**	**SAME**	**LUSHOTO**
L. Lokissa	A. Shoo	G. Kissima	J. Mzoo
R. Swai	F. Moshi	Mr. Marialle	Mr. Chandenda
F. Mboye			
Mr. Macha			
F. Moshi			
MIPANGO ARDHI			
F. Moshi	Ms. Maringo	G. Kissima	Mr. Mshana
F. Mboye	Mr. Kiwelu	Mr. Mallya	
UIMARISHAJI VIKUNDI NA JINSIA			
Grace Mghase	W. Salum	S. Mfinanga	B. Shemdoe
MASOKO			
L. Lokissa	NIL	S. Mfinanga	B. Shemdoe

WASHIRIKA WA TIP

Umwagiliaji:

- Bw. Lyimo – Mchora Ramani
- Bw. Lelo – Mchora Ramani
- Bw. Marandu – Afisa Kilimo
- Bw. Swai – Mtaalamu wa Ujenzi

Mipango Ardhi:

- Bw. Kombo – Mtaalamu wa GIS
- Bw. F. Mlenge – Mhadhiri Chuo Kikuu cha Ardhi
- Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Ardhi

Inaenelea uk. wa 4

MAJIRA YA TIP

UKARABATI WA MFUMO WA UMWAGILIAJI WA CHEKERENI WERUWERU

Mradi wa umwagiliaji wa Chekereni Weruweru upo kusini mwa mji wa Moshi katika ukanda wa chini wa mkoa wa Kilimanjaro, Tanzania. Mradi huu mulianzishwa na kuendelezwa na wakulima wenyewe. Katika miaka ya 1970 Serikali ya Tanzania iliwapa msaada kwa kuwajengea banio pamoja na lango. Eneo zima lililopo katika mfumo huu wa umwagiliaji ni hekta 145 japokuwa ni hekta 25 tu zinazotumika kwa sasa katika kilimo cha umwagiliaji. Mihindi na mpunga ndiyo mazao makuu yanayolimwa sana katika mfumo huu. Kikundi cha watumia maji kina wastani wa wanachama 200.

Kwa kufuatia mapendekezo ya TIP katika shuguli ambazo zingefanyika, bajeti kwa ajili ya ukarabati wa mfumo mzima ilitengenezwa na baadaye ilipelekwa katika Ubalozi wa Japani nachini Tanzania kwa ajili ya msaada wa kifedha kupitia maradi wa GAGRP(Grant Assistance for Grass Roots Project)

Ubalozi wa Japani uliipitisha bajeti mwezi Octoba 2002 baada ya kufanyiwa marekebisho kadhaa. Hata hivyo bajeti iliyopitishwa na kutolewa ilikuwa inalenga upande wa ujenzi wa mfereji tuu. Kwa kutumia utaratibu wake wa kawida wa kufanya kazi, TIP ilitafuta wafadhili wengine ili iweze kukamilisha kazi zilizobakia za uhifadhi wa udongo na uimarishaji vikundi. Jumla ya pesa zilizotolewa na Ubalozi wa Japani ni Tsh. 30,000,000/=.
Kipindi kizima cha ujenzi ni muda wa mwaka mmoja.

Tokea tarehe 30/06/2003 kazi ya ujenzi wa mradi imefikia kiwango cha asilimia 50%. Mradi huu unatekelezwa na TIP kwa kushirikiana na wadau ambapo wadau wa mradi huchangia nguvu kazi na TIP huchangia utaalamu. Mhandisi wa TIP ndiye msimamizi wa utekelezaji wa mradi kwa ujumla akishirikiana na mtaalamu wa umwagiliaji wa wilaya ya Arumeru Bw. Ronald Swai.

Matokeo yanayotegemewa kuwepo ni uongezekaji wa maji, usimamizi mzuri wa maji na ongezeko la uzalishaji litaihakikishia jamii kuwepo kwa chakula. Matokeo mengine ni utunzaji wa mazingira katika mto Kiladeda na maeneo ya mfereji mkuu.

Ujenzi wa langa la maji katika mto Kiladeda

Barua za wasomaji

Tunakaribisha maoni, mapendekezo, hadithi, na fikra yoyote yenye kuelimisha jamii ili tuchapishe.
Tuandikie ukionyesha jina kamili na anwani kwa:
TIP, Box 8909 Moshi,Kilimanjaro

SHUKRANI!!!

Shukrani za pekee ziwaendee :

NOVIB, UBALOZI WA JAPANI, UBALOZI WA UHOLANZI NA SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA (UNDP)

Kwa ufadhili wa shughuli za **TIP**

Shirika la Uboreshaji Kilimo cha Umwagiliaji wa Mifereji Asili na Mmazingira ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa tangu 1999. Hata hivyo shirika hili lisilo la kiserikali lili-undwa mnamo mwaka 1988, wakati ambao TIP lilianzishwa kama mpango wa Uboreshaji wa Umwagiliaji chini ya waasisi wa shirika la Maendeleo la Uholanzi (Netherlands SNV). TIP inashirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweza kuwafikia kwa urahisi walengwa ambao ni wakulima wa maeneo ya um-wagiliaji kwa mifereji ya asili. Malengo ya TIP ni kuboresha na kuinua viwango vya maisha ya jamii za maeneo ya Tanzania yenye ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili kuhifadhi maji na udongo, kustawisha misitu na maeneo ya vyanzo vya maji nchini Tanzania

TIP NI MSAADA WAKO WA MAENDELEO

Malengo makuu mnne:

- Usimamizi madhubuti na uhusiano wa kijinsia
- Kuhifadhi ardhi na maji
- Kuboresha mifereji ya asili
- Wakulima na Masoko

Wasiliana nasi Katika ofisi zetu Moshi

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi katika ofisi yetu ya Moshi

S.L.P 8909, Moshi - Kilimanjaro
SIMU: 027 53025/54232
FAX: 027 51124
E-mail: tip@eoltz.com

Inatoka uk. 2

Uimarishaji Vikundi na Jinsia
- Bi. S. Kilala

Masoko
- Chuo Cha Ushirika Moshi Tawi la Kilimanjaro
- FAIDA –BDS
- Bw. H. Lema – ENVIROCARE

Utawala wa Fedha
- Chuo cha Ushirika Moshi – Tawi la Kilimanjaro

Mwendelezo wa Mtandao wa TIP

TIP itaendelea kutumia mtandao wake katika kutekeleza kazi zake kwa wakulima waishio maeneo ya uten-daji kazi wa TIP. Na pia itaendelea kutoa mafunzo bora kwa wafanyakazi wake ili kuendelea kuwa bora katika utendaji kazi.

KAZI ZA TIP KWA IDARA

TIP inafanya kazi katika Wilaya nne kwa kushirikiana na wafanyakazi wa halmashauri wa idara ya um-wagiliaji, kilimo na ustawi wa jamii. Wafanyakazi hao ni;

i). Afisa Umwagiliaji wa Wilaya ambaye ni Meneja wa TIP wa wilaya
ii). Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ambaye ni Afisa Jinsia na Uimarishaji wa vikundi vya TIP
iii). Wataalamu wa Umwagiliaji
iv). Wataalamu wa Mipango Ardhi
v). Wakulima vichocheo

Shughuli katika kila idara zinafanywa kwa muongozo wa azma ya TIP.
Shughuli zenyewe ni;

- Uimarishaji Vikundi Na Jinsia
  - Upembuzi Yakinifu
  - Usajilishaji wa vikundi
  - Kufundisha wakulima miongozo ya vikundi (kama; uongozi, uwekaji kumbu-kumbu,mawasiliano n.k)
  - Kufundisha vikundi vya wakulima elimu ya jinsia
  - Kuwezesha wizara ya mafunzo kwa wakulima
  - Kuwafundisha wakulima kuanzisha umoja wa kuweka na kukopa
  - Uwezeshaji na uandikishaji wa vyama vya ushirika

- Uimarishaji mifereji ya asili
  - kufundisha wakulima matumizi bora ya maji
  - upimaji na usanifu wa vijengo vya mumwagiliaji
  - ujenzi wa vijengo vya umwagiliaji
  - ujenzi wa mifereji
  - kuoredhesha vikundi vya umwagiliaji maji
  - kupima wingi wa maji
  - uanzishaji kamati ya bonde.

- Hifadhi ya Ardhi
  - Mafunzo ya mbinu/njia mbalimbali za kuhifadhi ardhi na maji kwa wataalamu na wakulima vichocheo
  - Mafunzo ya uandaaji vitalu vya miche
  - Ujenzi wa matuta (fanya juu,matuta ya ngazi n.k)
  - mafunzo ya ngozi na ushirikishwaji katika mipango ardhi

- Masoko Na Vikundi Vya Uzalishaji
  - Uundaji wa vikundi vya uzalishaji na masoko
  - mfunzo ya biashara, utaalamu wa kilimo, upimaji wa udongo, na kufanya majaribio
  - mafunzo ya uhifadhi wa mavuno
  - ziara za mafunzo
  - kuwezwsha utafiti wa masoko kwa wakulima

Shughuli zingine zinazofanyika ofisi kuu
- mafunzo katika nyanja mbalimbali kwa wafanyakazi wa TIP
- tathimini ya miradi mbalimbali ya vikundi vya umwagiliaji
- kuwezesha wakulima kuhudhuria sikukuu ya wakulima
- kuandaa vijarida vya wakulima
- ukusanyaji wa takwimu
- uchoraji wa ramani za maeneo ambayo TIP hufanya kazi

Walengwa wa shughuli za TIP ni wakulima wadogo walioungani kwenye vikundi vya umwagiliaji.